**Journal of Kiswahili and Other African Languages**
Vol. 3 No. 1 (2025): ISSN (Online): 2958-4914
DOI: https://doi.org/10.58721/jkal.v3i1.997


# Sababu za Kupungua kwa Matumizi ya Majina ya Asili Nchini Tanzania: Mifano Kutoka Ginantuzu Lahaja ya Kisukuma

**Njana Masanja**
*The Mwalimu Nyerere Memorial Academy, Tanzania*

**Uwasilishaji wa Makala**
*Kupokelewa: 2024-12-30*
*Kurekebishwa: 2025-04-12*
*Kukubaliwa: 2025-04-14*
*Kuchapishwa: 2025-04-15*

***Maneno Muhimu***
Athari
Ginantuzu
Kupungua
Majina ya Asili

**Jinsi ya Kurejelea Makala:**
Masanja, N. (2025). Sababu za Kupungua kwa Matumizi ya Majina ya Asili Nchini Tanzania. Mifano Kutoka Ginantuzu Lahaja ya Kisukuma. *Journal of Kiswahili and Other African Languages*, *3*(1), 29-36.

*Copyright © 2025*
CC BY NC SA

**Ikisiri**
Miaka ya hivi karibuni majina ya asili yamekuwa yakikabiliwa na changamoto ya kupotea kwa kasi isiyo kifani hasa kwa vijana nchini Tanzania. Makala hii imechunguza sababu za kupungua kwa matumizi ya majina ya asili katika koo za Ginantuzu, mojawapo ya lahaja za Kisukuma. Makala imeongozwa na baadhi ya maswali. Maswali hayo ni: Kwa nini majina ya asili yanapungua kila kukicha nchini Tanzania? Nini sababu za kupungua kwa matumizi ya majina ya asili hasa kwa vijana? Nini athari kwa jamii iwapo majina ya asili yakipotea? Data za makala hii zilikusanywa kwa mbinu ya ushuhudiaji, mahojiano, hojaji na mapitio ya nyaraka za maktabani, makavazi na mitandaoni. Makala ilitumia mkabala wa kitaamuli. Matokeo ya makala yameonesha kuwa, sababu za kupungua kwa matumizi ya majina ya asili katika koo za Ginantuzu ni mwingiliano wa ndoa katika familia, kuingia kwa dini ya Ukristo, kuporomoka kwa maadili kwa vijana, uhamiaji, kukosa umaarufu kwa majina ya asili, kasumba za ustaarabu kwa vijana, baadhi ya majina kupitwa na wakati, kukosa elimu kuhusu majina ya asili, na utandawazi. Aidha, makala pia inaonesha kuwa athari za kupotea kwa majina ya asili ni: kupoteza utambulisho wa jamii, kupoteza utamaduni, na kuhafifisha falsafa asilia za Ginantuzu zilizofumbatwa katika majina hayo. Makala inapendekeza kuwa wanajamii wanapaswa kupewe elimu kuhusu maana ya majina ya asili, pamoja na umuhimu wa kuyatumia. Hii itakuwa njia mwafaka ya kuhifadhi utamaduni, falsafa na historia ya jamii ya Ginantuzi kupitia majina ya asili.

## Utangulizi

Kila kiumbe na hali hupewa jina na binadamu ili kusaidia utambuzi wa haraka wa kile kinachorejelewa. Majina ya asili ni majina ambayo chimbuko, historia na maana yake hutokana na vigezo, taratibu na kanuni zilizobeba maana kulingana na mila, desturi na utamaduni wa jamii husika. Nyangaywa (2013) anasema kuwa, majina ya asili katika jamii nyingi hutokana na lughamama ambazo hutumika katika kuwasiliana na pia maana za majina hayo hujulikana na jamii husika. Kwa maana hiyo basi, majina ya asili hutolewa katika familia baada tu ya mtoto kuzaliwa. Majina hayo hutolewa kulingana na mila na desturi za jamii husika kwa kurithi kutoka kwenye majina ya ukoo, majina ya utani au matukio yaliyojitokeza katika jamii husika. Muzale (1998) anasema kuwa, utoaji wa majina ya asili kwa mtoto ni tukio muhimu sana katika jamii za Kiafrika. Mbiti (1990) anaongeza kuwa, katika imani za Kiafrika majina yana athari katika tabia ya mtoto, afya ya mtoto, mwenendo, mafanikio na hata maendeleo ya mtoto baadaye.

Kimsingi suala la dhana ya majina kwa watu na vitu ni mada ambayo imewavutia wanaisimu wengi duniani kote. Wataalamu kama Zakaria (2020), Masanja (2019), Anusa (2016), Mapunada (2014), Azael (2013), Kategela (2013), Jonas (2013) na Nyangaywa (2013) walijikita kuchunguza majina huku kila mmoja akichunguza vipengele kulingana na malengo ya utafiti wake. Watafiti wengine waliochunguza majina ni Elihaki (2012), Olenyo (2011), Buberwa (2010), Musere (2010) na Manyasa (2009). Wataalamu kama Elihaki (2012) na Buberwa (2010) nao hawakuwa nyuma kuchunguza majina.

Baadhi ya watafiti kama Masanja (2019), Anusa (2016), Azael (2013), Jonas (2013) na Nyangaywa (2013) walijikita kuchunguza kipengele cha maana ya majina ya asili na vipengele vingine katika jamii zao. Mapunda (2014) aliangalia majina ya utani wanayopewa wahadhiri katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Naye Kategela (2013) alichuchunguza matumizi ya majina ya asili ya familia na utambulisho wa jamii ya Wanyakyusa. Mbiti (1990) alijikita zaidi kuangalia dini za Kiafrika na falsafa ya uteuzi wa majina.

Uchuguzi wa Zakaria (2020) ulionesha kuwa, kiwango cha matumizi ya majina ya Kiswahili jijini Dar es Salaam ni asilimia 26.25 ya majina yote yaliyokusanywa katika utafiti wake. Aidha, kiwango cha matumizi ya majina kutoka lugha zingine ni asilimia 73.75 ya majina yote yaliyokusanywa katika utafiti huo. Utafiti huu ulitusaidia kuibua ari katika uandishi wa makala hii kwani majina ya Kiswahili yalikuwa na asilimia chache iliyoashiria kupungua kwa majina ya Kiswahili jijini Dar es Salaam.

Mapunda (2014) katika utafiti wake alichunguza majina ya utani wanayopewa wahadhiri na wanafunzi wao katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Matokeo ya utafiti wake yalionesha kuwa, majina mengi ya utani wanayopewa wahadhiri na wanafunzi wao yanaakisi tabia ya kukubalika au kutokubalika kwa wanafunzi wao kitabia na kitaaluma katika masomo wanayofundisha. Matokeo ya utafiti huu yanatuonesha kuwa, majina ya watu katika jamii hutoa utambulisho wa mtu husika. Mchango wa utafiti huu unaunga mkono hoja iliyopo katika kuchunguza sababu za kupungua kwa majina ya asili ya Ginyantuzu.

Gray (1999) na Kalkanova (1999) wanaeleza kwamba jina linaweza kutumika kumwakilisha mtu au jamii. Jina linaweza kuonesha uhusiano wa kijamii pamoja na kutunza hadhi ya jamii. Kutokana na matokeo ya mapitio ya wanaisimu hapo juu imedhihirisha kuwa, utoaji wa majina ya watu katika jamii nyingi za Kiafrika haufanyiki kiholela bali huzingatia taratibu na kanuni fulani zilizobeba maana kulingana na mila na desturi za jamii hiyo. Hoja hii inaungwa mkono na Ota (2002) anayesema kuwa, majina ya asili katika jamii za Kiafrika hayatolewi kiholela bali hufumbata kanuni mahususi zinazozingatia utamaduni wa jamii husika. Katika imani nyingi za Kiafrika na duniani kote kwa ujumla, majina ni muhimu sana. Jina ni zaidi ya neno linalomtambulisha mtu mmoja na mwingine. Rey (1995), Rugemalira (2005), na Koigi (2008) wanaeleza kuwa, jina husaidia katika utambuzi wa mtu kibinafsi na kirasmi, kijamii, kiutamaduni na hata kiuchumi. Pia, jina hilo humtambulisha mtu eneo analotoka, huashiria tabia yake, sifa zake, imani na fikra zake. Rugemalira (2005) katika utafiti wake anabainisha kuwa, majina na lugha nyingi za Kibantu yanafifia na hata kuwa hatarini kupotea au kutoweka. Hii inatokana na watu hasa vijana kutojua thamani iliyobebwa na majina ya lugha hizo katika nyanja mbailmbali. Utafiti huu ulichochea haja ya kwenda uwandani ili kutafiti sababu za kupungua kwa matumizi ya majina ya asili katika koo za Ginantuzu.

Ingawa kipengele cha majina kinaonekana kushughulikiwa na wanaisimu mbalimbali kama walivyotajwa hapo juu, tafiti zao zilimakinika zaidi katika kuchunguza majina ya watu na mahali wala hazikushughulikia kipengele cha sababu za kupungua kwa matumizi ya majina ya asili katika

jamii. Ili kuziba pengo hili lengo, makala hii inabainisha sababu za kupungua kwa matumizi ya majina ya asili katika koo za Ginantuzu.

**Mbinu za Utafiti**

Data za makala hii zilikusanywa katika mkoa wa Simiyu katika wilaya ya Bariadi na Itilima. Jumla ya kata sita zilifanyiwa uchunguzi. Kata hizo ni Sapiwi, Nkololo na Bariadi zilizoko Wilaya ya Bariadi na Bumera, Lagangabilili, na Lugulu zilizoko Wilaya ya Itilima. Jumla ya vijiji kumi vilipitiwa na mtafiti ambavyo ni Igegu, Bariadi, Sapiwi, Nkololo, Lugulu, Bulolambeshi, Kidinda, Byuna, Lagangabilili na Bumera. Mbinu zilizotumika katika ukusanyaji wa data ni mapitio ya nyaraka maktabani, makavazi na mitandaoni. Mbinu nyingine zilizotumika kukusanya data za utafiti ni ushuhudiaji, mahojiano na hojaji. Uwasilishwaji ulifanywa kwa njia ya maelezo kwa kiasi kikubwa na majedwali kwa kiasi kidogo. Jumla ya watoataarifa arobaini (40) walipewa dodoso na kuzijaza. Watoataarifa thelathini na nane (38) walisailiwa na kufanya kuwa na sampuli ya watu sabini na nane (78). Usampulishaji nasibu ulitumika kupata sampuli hiyo. Wastani wa watu 8 kwa kila kijiji walipatikana kwa uwiano sawa wa kijinsia. Watoataarifa walioteuliwa waliwekwa katika makundi makuu mawili ambayo ni kundi la wazee arobaini (40) wa jinsia zote wenye umri wa kuanzia miaka 55- 85 katika uwiano sawa wa kijinsia. Kundi la pili lilikuwa la watu thelathini na nane (38) wa jinsia zote wenye umri wa kuanzia miaka 25–54 katika uwiano sawa wa kijinsia. Ama kuhusu mkabala, makala hii ilitumia kwa kiasi kikubwa mkabala wa kitaamuli na kitakwimu kidogo katika uchanganuzi wa data.

**Matokeo ya Utafiti**

Matokeo ya utafiti huu yaligawanywa katika sehemu mbili: kwanza, sababu za kupungua kwa majina ya asili, na pili, athari za kupotea kwa majina ya asili ya Ginantuzu.

***Sababu za Kupungua kwa Matumizi ya Majina ya Asili katika Koo za Ginantuzu***

Matakeo ya uchambuzi yalionesha kwamba, matumizi ya majina ya asili katika koo za Ginantuzu yameanza kupungua kutokana na sababu mbalimbali. Sababu za kupungua kwa matumizi ya majina ya asili ya koo za Ginantuzu kuwa ni: mwingiliano wa ndoa katika familia, kuingia kwa dini ya Ukristo, kuporomoka kwa maadili kwa vijana, uhamiaji, kukosa umaarufu kwa majina ya asili, kasumba za ustaarabu kwa vijana, baadhi ya majina kupitwa na wakati, kukosa elimu juu ya majina ya asili na utandawazi. Muhtasari wa watoa taarifa umebainishwa kitakwimu katika jedwali Na. 1:

*Jedwali la 1: Sababu za kupungua kwa matumizi ya majina ya asili katika koo za Ginantuzu*

| S/N | Idadi ya watafitiwa | Asilimia | Sababu |
|---|---|---|---|
| 1 | 18 | 23.07% | Mwingiliano wa ndoa katika familia |
| 2 | 12 | 15.4% | Kuingia kwa Ukristo |
| 3 | 10 | 12.82% | Kuporomoka kwa maadili kwa vijana |
| 4 | 08 | 10.26% | Uhamiaji |
| 5 | 07 | 8.97% | Kukosa umaarufu kwa majina ya asili |
| 6 | 07 | 8.97% | Kasumba za ustaarabu kwa vijana |
| 7 | 06 | 7.7% | Baadhi ya majina kupitwa na wakati |
| 8 | 05 | 6.41% | Kukosa elimu juu ya majina ya asili |
| 9 | 05 | 6.41% | Utandawazi |
| JUMLA | 78 | 100% | |

Ufafanuzi zaidi wa sababu hizi umeelezwa hapa chini kwa undani.

Journal of Kiswahili and Other African Languages
Vol. 3 No. 1 (2025): ISSN (Online): 2958-4914
DOI: https://doi.org/10.58721/jkal.v3i1.997


***Mwingiliano wa Ndoa katika Familia***

Mwingiliano wa ndoa katika kuoana ni mojawapo ya sababu za kupungua kwa matumizi ya majina ya asili katika koo za Ginantuzu. Watoataarifa 18 kati ya 80 sawa na asilimia 22.07 waliohojiwa walieleza kuwa, vijana wengi katika koo za Ginantuzu wameoa au wameolewa na makabila tofauti na Ginantuzu. Watoataarifa hao walifafanua kuwa, suala la kuoana na jamii tofauti limezua mgongano na mwingiliano wa kiutamaduni unaoathiri taratibu za utoaji na utumiaji wa majina ya asili katika koo za Ginantuzu. Aidha, hapo zamani jukumu la kutoa jina kwa mtoto anayezaliwa katika koo za Ginantuzu lilikuwa pande zote mbili, yaani upande wa baba na upande wa mama. Baada ya mwingiliano wa ndoa, baadhi ya familia waliamua kuwapa watoto majina yasiyo ya Ginantuzu. Hivyo, mwingiliano wa ndoa katika familia ni sababu iliyosababisha kupungua kwa matumizi ya majina ya asili katika koo za Ginantuzu.

***Kuingia kwa Ukristo***

Kuingia kwa dini ya Kikristo kutoka Magharibi ni miongoni mwa sababu za kupungua kwa matumizi ya majina ya asili katika koo za Ginantuzu. Watoa taarifa 12 kati ya 80 ambao ni sawa na asilimia 15.4 walieleza kuwa, ujio wa dini ya Kikristo umeleta imani mpya. Imani hii imewaathiri baadhi ya watu katika kutumia majina ya asili hasa yale yenye fasili hasi. Mmoja wa watoataarifa aliyekuwa mfuasi wa dini ya Kikristo katika mafundisho yao alisema, ''Majina ya asili tunayotumia ni ya kipagani ambayo yamefungamanishwa na miungu ya mababu pamoja na mizimu. Hivyo, tunapoamua kumfuata Kristo hatuna budi kuachana na majina ya asili na kuchukua majina ambayo yana uhusiano wa moja kwa moja na Mungu”

Kulingana na maelezo ya watoataarifa ni dhahiri kuwa, kuingia kwa Ukristo ni sababu iliyopelekea kupungua kwa matumizi ya majina ya asili katika koo za Ginantuzu. Baadhi ya wafuasi wa dini ya Kikrito waliamua kuachachana na majina ya asili na kuchukua majina ya Kikristo. Maamuzi ya kuachana na majina ya asili kulipelekea kupungua kwa matumizi ya majina ya asili katika koo za Ginantuzu. Wakristo hawa walijitenga moja kwa moja na utambulisho, utamaduni na, misingi ya jamii na kuhafifisha falsafa asilia za Kinyantuzu zilizofumbatwa katika majina hayo kwa kuwa hayatumiwi tena.

***Kuporomoka kwa Maadili kwa Vijana***

Kuporomoka kwa maadili kwa vijana ni sababu nyingine ya kupungua kwa matumizi ya majina ya asili katika koo za Ginantuzu. Watoataarifa 10 kati ya 80 ambao ni sawa na asilimia 12.82 waliofikiwa na mtafiti kwa njia ya mahojiano walisema kuwa, baadhi ya vijana wa Ginantuzu wamejipa jukumu la kutoa majina ya asili kwa watoto wanaowazaa. Mmoja wa watoataarifa alieleza kwamba, ''Hapo mwanzo jukumu la kutoa jina kwa mtoto aliyezaliwa halikuwa la mzazi wa mtoto huyo bali lilikuwa jukumu la wazazi wa wazazi wa mtoto kama babu, bibi, mjomba, shangazi au ndugu mwingine wa karibu.'' Mmoja wa watoataarifa alieleza kuwa, hali ya kujichukulia madaraka ya kutoa jina kwa watoto wao haikufanywa na vijana wote bali ilianza kufanywa na wachache. Baadaye watu hao wakaongezeka na kuyafanya majina ya asili kupungua kwa kiasi kikubwa.

Kulingana na utafiti ilibainika kuwa katika maadili na desturi za Ginantuzu ni makosa kwa mzazi wa mtoto kutoa jina la mtoto wake mwenyewe. Mzazi wa mtoto akiwa mbali na wazazi wake, itamlazimu kufanya mawasiliano kwa njia yoyote na wazazi au ndugu wa karibu ili apate jina la kumpatia mtoto huyo. Kwa kuwa jukumu la kutoa jina kwa mtoto aliyezaliwa limechukuliwa na wazazi wa mtoto, hali hii katika maadili na desturi za Ginantuzu inadhihirisha kuporomoka kwa maadili kwa vijana. Hali hii inasababisha kupungua kwa matumizi ya majina ya asili katika koo za Ginantuzu.

Kuporomoka kwa maadili kwa wazazi hawa kumesababishwa na jinsi wanavyouelewa ulimwengu wao tofauti na ilivyokuwa hapo awali katika koo za Ginantuzu.

***Uhamiaji***

Uhamiaji ni miongoni mwa sababu za kupungua kwa matumizi ya majina ya asili katika koo za Ginantuzu. Watoa taarifa 8 kati ya 80 ambao ni sawa na asilimia 10.26 walieleza kuwa, hapo mwanzo, watu katika koo za Ginantuzu waliishi kwa pamoja kama jamii moja. Boma moja liliweza kuwa na watu zaidi ya sabini likiwa na mzee mmoja. Baada ya hali ya hewa kubadilika na kuwa mbaya, njaa ilianza kuingia katika maeneo husika. Familia zilianza kukosa chakula na malisho ya mifugo. Watu waliamua kutoka na kwenda sehemu mbalimbali kwa ajili ya kutafuta chakula na malisho ya mifugo yao. Huko walikoenda nako waliendelea kuoana na jamii zingine ambazo si za Ginantuzu. Kwa kufanya hivyo, hata zile taratibu za kutoa majina ya asili kwa watoto wao zilipungua.

Kulingana na maelezo ya watoataarifa ni dhahiri kuwa, uhamiaji ni sababu iliyopelekea kupungua kwa matumizi ya majina ya asili katika koo za Ginantuzu kwani huko walikohamia walioana na jamii zingine ambazo si za Ginantuzu. Majina ya asili yalipungua na majina yasiyo ya asili yakachukua nafasi. Aidha, wahamiaji hao waliingiliana na jamii tofauti jambo lililoathiri hata taratibu za utoaji wa majina kutoka katika misingi ya koo za Ginantuzu. Watoto waliozaliwa ambao hawapewa majina ya asili pia hawakuweza kuwarithisha watoto wao na vizazi vyao majina hayo ya asili. Hali hii ilichangia katika kupungua kwa matumizi ya majina ya asili ya jamii ya Ginantuzu.

***Kukosa Umaarufu kwa Majina ya Asili***

Kukosa umaarufu kwa baadhi ya majina ya asili ni sababu nyingine iliyoibuliwa na watoataarifa katika data zao. Watoataarifa 7 kati ya 80 sawa na asilimia 8.97 waliohojiwa walieleza kuwa, wapo watu katika koo za Ginantuzu walipenda kuwapa watoto wao majina ya asili. Ila kukosekana kwa umaarufu kwa majina hayo kuliwavunja moyo kwa njia moja au nyingine. Hali hiyo iliwapelekea wazazi kuwapa watoto wao majina ya kigeni kwa sababu majina ya asili yamekosa umaarufu. Katika imani, mila na desturi za Ginantuzu, wanajamii wanaamini kuwa jina la mtoto lina athari fulani kwa mtoto. Hivyo, kumpa mtoto jina la asili la mtu mwenye taswira hasi ni kumtabiria mabaya mtoto wake.

Kukosa umaarufu kwa baadhi ya majina ya asili ni sababu iliyopelekea kupungua kwa matumizi ya majina ya asili katika koo za Ginantuzu. Ni dhahiri kuwa, hapo nyuma watu walipendelea sana kuwapa watoto wao majina ya asili hasa majina yenye umaarufu kama tajiri, shujaa, kiongozi shupavu, hata mwenye busara na hekima. Kwa kufanya hivyo jina lenye sifa hizo lilipendwa na kutumiwa na wanaukoo wengi kwa imani kuwa, watoto waliowapa majina hayo wataiga tabia na matendo ya mwanzilishi wa jina hilo. Kwa sasa, baadhi wa wanajamii hawayaonei fahari majina hayo tena kwani kuwawajui watu hao maarufu wa enzi hizo, na hawawezi kujinasibisha nao. Badala yake wanapendelea kujinasibisha na watu maarufu wa enzi za kisasa ambao si lazima wawe wa jamii ya Ginantuzu. Aidha, baadhi ya wanajamii hayaenzi majina ya asili yenye taswira hasi. Haya yamesababisha kupungua kwa matumizi ya majina ya asili katika jamii hii.

***Kasumba za Ustaarabu kwa vijana***

Kasumba za ustaarabu ni sababu iliyoibuliwa na watoa taarifa kuhusu kupungua kwa matumizi ya majina ya asili katika koo za Ginantuzu. Watoataarifa 7 kati ya 80 sawa na asilimia 8.97 walisema kuwa, baadhi ya watu katika jamii hasa wasomi wanapenda sana kuiga majina ya kigeni na kuona majina ya asili hayana maana. Watoataarifa walieleza kuwa, hawapendi kutumia majina ya asili kwa kuwa hawapendi kujulikana kuwa wanatoka katika kabila gani kwani kuna makabila

yaliyostaarabika na mengine bado. Mtafiti alimuuliza mtoataarifa swali, ''Kwa nini mtoto wako uliimwita Moses?'' Mtoa taarifa alisema, aliamua kuachana na majina ya asili yasiyoakisi ustaarabu na kumwita mtoto wake Moses kwa sababu kwanza, Moses ni jina maarufu kama kiongozi wa wana wa Israel. Mtafiti alimwambia asome Biblia katika kitabu cha *Kutoka 2: 1-10* inasemaje kuhusu jina Moses? Mtoataarifa alisoma na kubaini kuwa maana ya jina Moses ni *Kuokotwa baharini*. Je, mtoto wako Moses umemwokota baharini? Na kama ulimwokota kwa nini usimwite jina hilo kwa lugha yako mama kuwa ni *Masolwa?* Mtafiti alihoji. Mwisho wa mahojiano mtoataarifa alikiri kuwa ni kasumba na kusema kuwa elimu kuhusu majina inahitajika sana kwa kila mmoja wetu. Hivyo, kasumba za ustaarabu ni sababu iliyopelekea kupungua kwa matumizi ya majina ya asili katika koo za Ginantuzu. Baadhi ya watu wanafuata mkumbo bila kuwa na uelewa juu ya majina na kujikuta wameacha misingi iliyowekwa juu ya majina ya asili.

***Baadhi ya Majina Kupitwa na Wakati***

Baadhi ya majina kupitwa na wakati ni sababu iliyoibuliwa na watoa taarifa kuhusu kupungua kwa matumizi ya majina ya asili katika koo za Ginantuzu. Watoataarifa 6 kati ya 80 sawa na asilimia 7.7 waliofikiwa na mtafiti walisema kuwa, baadhi ya majina ya asili katika koo za Ginantuzu yamepitwa na wakati. Watoataarifa walieleza kuwa, ''Kuna haja gani ya kumpatia mtoto jina la ***Makoye*** lenye maana ya matatizo kwa sababu lilikuwa jina la babu yake aliyezaliwa kwa matatizo kipindi hicho?'' Enzi za majina kama haya zimepitwa na wakati. Ulimwengu wa leo si ulimwengu wa jana. Hivyo basi, baadhi ya majina kupitwa na wakati ni sababu iliyopelekea kupungua kwa matumizi ya majina ya asili katika koo za Ginantuzu.

***Kukosa Elimu Kuhusu Majina ya Asili***

Kukosa elimu kuhusu majina ya asili katika koo za Ginantuzu ni sababu iliyopelekea kupungua kwa matumizi ya majina ya asili katika koo za Ginantuzu. Watoataarifa 5 kati ya 80 sawa na asilimia 6.41 walisema kwamba, majina mengi ya asili waliyowapa watoto wao hawajui maana yake. Wanapouliza kwa wakubwa wao kuwa yana maana gani, wanaambiwa ni majina ya ukoo tu ila maana yake hawaitambui. Mtafiti alichukua majina 12 ya asili na kuuliza maana yake kwa vijana na wazee. Majina 4 tu ndio yalipata maana yake kutoka kwa wazee.

Hali hii imedhihirisha kuwa, kukosa elimu kuhusu majina ya asili kwa jamii ni sababu iliyopelekea kupungua kwa matumizi ya majina ya asili katika koo za Ginantuzu. Matokeo yalionesha kuwa elimu kuhusu majina ya asili imepungua kwa wengi. Jamii ya sasa imeathiriwa na ulimwengu wa sasa, hivyo kupelekea wanajamii ya kisasa kupendelea majina ya kisasa kuliko yale ya kiasili.

***Utandawazi***

Utandawazi ni sababu za kupungua kwa matumizi ya majina ya asili katika koo za Ginantuzu. Hayo yameibuliwa na watoataarifa 5 kati ya 80 sawa na asilimia 6.41 waliosema kwamba, ''Siku hizi majina mengi mazuri na yenye umaarufu tunayatoa katika mitandao ya kijamii kwa kuangalia watu maarufu na waliofanya makubwa'' Mengi ya majina hayo kutoka mitandaoni ni ya watu mashuhuri kama Washington, Lopez, Ronaldo, Madona, Serena, Sara, Ester na Moses. Njozi hii ya kuita majina ya watu maarufu imetawala sana katika koo za Ginantuzu. Hivyo basi, utandawazi ni sababu iliyopelekea kupungua kwa matumizi ya majina ya asili katika koo za Ginantuzu. Hivi sasa jamii inaamini kuwa, kuwapatia watoto wao majina ya watu maarufu, kutawapelekea kuwa watu wakubwa na maarufu siku moja, sawasawa na wamiliki wa majina hayo. Utandawazi umewavuta wengi na kujikuta wakibeza majina yao ya asili na kuamini majina ya mitandaoni ambayo hayaakisi utamaduni wao.

***Athari za Kupotea kwa Majina ya Asili ya Ginantuzu***

Data zilizotolewa zimedhihirisha kuwa, zipo athari kadha wa kadha iwapo majina ya asili ya Ginantuzu yatapotea. Baadhi ya athari hizo ni; kupoteza utambulisho wa jamii, kupoteza utamaduni wa kijamii, kupoteza misingi ya jamii husika na kuhafifisha falsafa asilia za Ginantuzu zilizofumbatwa katika majina hayo kwak uwa hayatumiwi tena. Ili kuweza kudumisha matumizi ya majina asili katika koo za Ginantuzi, makala haya yanapendekeza kuwa wanajamii hasa vijana waeleimishwe kuhusu maana ya majina ya asili pamoja na umuhimu wa kuyatumia. Matumizi ya majina ya asili yatakuwa muhimu katika kuitambulisha jamii hii, na kuhifadhi utamaduni, falsafa na historia ya jamii. Hata hivyo, majina yaliyopitwa na wakati au yenye hulka hasi yanafaa kutupiliwa mbali au kuangaliwa upya ili yakubalike na wanajamii.

**Hitimisho**

Makala imeonesha kwamba, sababu za kupungua kwa matumizi ya majina ya asili katika koo za, Ginantuzu ni pamoja na: mwingiliano wa ndoa katika familia, kuingia kwa dini ya Kikristo, kuporomoka kwa maadili kwa vijana, uhamiaji, kukosa umaarufu kwa majina ya asili, kasumba za ustaarabu kwa vijana, baadhi ya majina kupitwa na wakati, kukosa elimu juu ya majina ya asili na utandawazi. Kuna umuhimu wa kutoa elimu kwa njia mbalimbali kwa jamii kuhusu maana ya majina ya asili pamoja na umuhimu wa kuyatumia ili kuitambulisha jamii na kuuhifadhi utamaduni, falsafa na historia ya jamii.

**Marejeleo**

Azael, R. (2013). *Maana ya majina ya asili katika jamii ya Kiuru*. Tasnifu ya Umahiri, (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dae es Salaam.

Anusa, H. J. (2016). *Maana za majina ya watu katika jamii ya Wayao*. Tasnifu ya Umahiri, (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Buberwa, E. (2010). *Investigating sociolinguistics aspect of place names in Ruhaya in North –Westerro Tanzania*, Master's Dessertaion, (Unpublished). University of Dar-es-Salaam.

Elihaki, Y. (2012). *Majina ya mahali katika jamiilugha ya Chasu*. Tasnifu ya Umahiri, (Hajachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Gray, T. M. (1999). *What's in a name? Some reflection on the Socialogy Annonymity*. http//web.ed/gt marx/a non.html.

Jonas, L. (2013). *Maana na misingi ya uteuzi wa majina ya watu katika lugha ya Kiha*. Tasnifu ya Umahiri, (Hajachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kalkanova, T. (1999). Sociology of Proper Names in Sophia since 1970. *International Journal of Sociology of Language, 1*(35), 83-98.

Kategela, R. (2013). *Matumizi ya Majina ya asili ya aamilia na atambulisho wa jamii ya Wanyakyusa*. Tasnifu ya Umahiri, (Hajachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Koigi. J. (2008). Literary Scene: What is in name? *Daily Nation*. Nairobi Medi Group, uk. 37.

Manyasa, J. (2009). *Investigating the basis of naming people in Kisukuma*. Tasnifu ya M.A. Isimu, (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Cha Dar –es- Salaam.

Mapunda, G. (2014). What do my students call me? Nicknaming of lecturers by students at University of Dar es Salaam. *Journal of Linguistics and Language in Education, 1*(8), 90- 107.

Masanja, N.T. (2019). *Uchunguzi wa Kisemantiki wa Majina ya Asili katika Ginantuzu*. Tasnifu ya Uzamivu, (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mbiti, S. (1990). *African Religion and Philosophy*. Heinemann Educational Books Inc.

Musere, J. (2010). *African Person Names Derived from African Pro*. llE line aArhicle. Com/2expert=Jonathan Musere.

Muzale H. R. T. (1998). "Linguistic and Socio-Cultural Aspects in Interlacustrine Bantu Names" University of Dar es Salaam. *Kiswahili Juzuu, 1*(61), 28-50.

Nyangaywa, M. (2013). *Uchunguzi wa Kisemantiki na Taratibu za Utoaji wa Majina ya Kijita*. Tasnifu ya Umahiri, (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Olenyo, M. M. J. (2011). ''What is in a name? An analysis of the semantics of Lulogooli personal names''. *International Journal of Humanities and Social Science*, *1*(20), 25-47.

Ota, O. (2002). *Edo Person Names and World View*. New Perspective in Edoed Studies, Nigeria.

Rey, A. (1995). *Essay on Terminology*. John Benjamin Publishing Company.

Rugemalira, J. M. (2005). *A Grammar of Runyambo*. LOT.

Zacharia, M. (2020). *Matumizi ya majina ya kiswahili Jijini Dar es Salaam, Nchini Tanzania*: *Uchunguzi kifani wa majina ya watu:* Tasnifu ya Umahiri, (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.